035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
   A. waraka
   B. barua maalum
   C. barua ya kiofisi
   D. Barua rasmi

   Jibu sahihi ni **D**

   **Katika karatasi ya majibu:**

   2. [A] [B] [C] [D] 12. [A] [B] [C] [D] 22. [A] [B] [C] [D] 32. [A] [B] [C] [D] 42. [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.
10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Dhana ya ufugaji wa wanyama sio ___1___ kwetu sisi binadamu hata kidogo. Tangu jadi ___2___ wanyama kwa manufaa yao ___3___. ___4___ faida hizo ni maziwa, nyama, ngozi na hata ___5___ tunayotumia kurutubisha mashamba yetu. ___6___, wanyama wengine hutumiwa katika shughuli za uchukuzi. Mtu ___7___ wanyama wa aina hii hujulikana kama ___8___. Hatupaswi kukiuka haki za wanyama; yafaa ___9___ ipasavyo ili waweze kutufaa.

1. A. wageni B. mgeni C. geni D. ngeni
2. A. tulikuwa tumewafuga B. tungekuwa tukiwafuga C. tulikuwa tukiwafuga D. tutakuwa tunawafuga
3. A. anuwai B. nyingi C. mingi D. furifuri
4. A. Kati ya B. Baadhi ya C. Kando ya D. Mbali na
5. A. samadi B. kemikali C. majani D. nyenzo
6. A. Licha ya hayo B. Mithili ya hayo C. Fauka ya hayo D. Dhidi ya hayo
7. A. wanaotunza B. anakotunza C. anaowatunza D. anayewatunza
8. A. sogora B. saisi C. mshenga D. mlisha
9. A. tuwatuze B. tuwahimize C. tuwalinde D. tuwasake

___10___ na shule ya Hekima, nilivutiwa sana na jinsi wanafunzi ___11___ lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Lugha yao ilipambwa kwa tasfida kama vile ___12___. Ni dhahiri kuwa walimu wa shule hii na wanafunzi wenyewe walikuwa wamefanya bidii kwa kuwa ___13___. Papo hapo, ___14___ kuinamia cha mvunguni ili nami ___15___ katika somo hilo. Moyoni nilijua kuwa penye nia pana njia.

10. A. Nilivyojiunga B. Nikajiunga C. Nilimojiunga D. Nilipojiunga
11. A. walivyotumia B. wanatumia C. waliotumia D. waliyotumia
12. A. Yakobo ni jogoo michezoni B. Mlevi alitembea uchi barabarani C. Shangazi yangu amezaa pacha D. Jirani alituacha mkono jana
13. A. Kinolewacho hupata B. Ukiona vyaelea vimeundwa C. Baada ya dhiki ni faraja D. Bidii ya mja haiondoi kudura
14. A. nilitia tashtiti B. nilikula mwata C. nilikata shauri D. nilikula mwande
15. A. niimarike B. niimarishe C. niimarikie D. niimarishie

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. **Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo.**
Vijana wale **wapole** wametuzwa **tena** leo.
A. Kivumishi, kiwakilishi
B. Kiwakilishi, kielezi
C. Kivumishi, kielezi
D. Kiwakilishi, kiunganishi.

17. Ni tashbihi ipi inayotoa maana ya **kuonekana vizuri au kuvutia**?
A. Chipua kama miche.
B. Chanua kama waridi.
C. Stawi kama mgomba.
D. Chipuka kama uyoga.

18. Chagua sentensi inayoonyesha kusudi la kutenda jambo.
A. Uzi huo ulivutwa sana ukakatika.
B. Aliwaletea wanawe zawadi akitoka safarini.
C. Vijana walimwona msanii wakafurahi sana.
D. Kijakazi anaingia jikoni akaoshe vyombo.

19. Sentensi '**Juma amekwenda kwake**' ina maana mbili. Zichague maana hizo.
A. (i) Amekwenda alikozaliwa.
(ii) Amekwenda alikotoka.
B. (i)Amekwenda alikotoka.
(ii) Amekwenda kusikojulikana.
C. (i) Amekwenda anakoishi.
(ii) Akwenda kwa mtu mwingine.
D. (i) Amekwenda alikozaliwa.
(ii) Amekwenda mbali na kwake.

20. **Nyoka** ni kwa kinyemere kama ilivyo **bata** kwa ____
A. kiyoyo
B. kipura
C. kinda
D.kidege.

21. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
Kobe huyo alipatikana palipokuwa na unyasi mrefu.
A. Kobe hao walipatikana palipokuwa na nyasi mrefu.
B. Makobe hayo yalipatikana palipokuwa na nyasi ndefu.
C. Makobe hao walipatikana palipokuwa na nyasi ndefu.
D. Kobe hao walipatikana palipokuwa na nyasi ndefu.

22. **Chagua sentensi mwafaka inayounganishi hizi.**
Chombo aliwalisha kuku. Kuku wenyewe walikuwa kizimbani.
A. Kizimbani walimlishia Chombo kuku.
B. Kuku walikula kizimbani kwa Chombo.
C. Kuku wa Chombo walilishwa kizimbani.
D. Chombo aliwalishia kuku kizimbani.

23. **Changamka** ni kwa **uchangamfu** kama ilivyo **cheka** kwa
A. mcheshi
B. kicheko
C. chekesha
D. cheshi.

24. **Ni methali gani inayoafikiana na maelezo haya?**
Haifai kuwadharau watu waliokusaidia hapo awali, huenda ukawahitaji tena.
A. Mkataa wengi ni mchawi.
B. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.
C. Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.
D. Usiache mbachao kwa msala upitao.

25. **Bainisha matumizi ya '-enye' katika sentensi ifuatayo.**
Mzee mwenye shamba hilo ni mkulima hodari.
A. Kuonyesha uhusiano.
B. Kuonyesha umilikaji.
C. Kuonyesha mahali.
D. Kuonyesha hali fulani.

26. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
Dege kuu linainamia wanawe.
A. Nyumba
B. Mvua
C. Mnazi
D. Mboga.

27. Shayiri, ufuta na mawele kwa jina moja ni
A. nafaka
B. vyakula
C. viungo
D. mtama.

28. **Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.**
Mwamu amemnunulia mzee jogoo.
A. Mwamu amemuuzia kijana jogoo.
B. Wifi amemwuzia kijana koo.
C. Wifi amemnunulia kijana mbarika.
D. Mwamu amemnunulia kijana kikwara.

29. Chagua maelezo yaliyo sahihi.
A. Lehemu ni kuunganisha vitu vya madini lakini rehemu kupewa neema na Muumba.
B. Kura ni uchaguzi wa kumpata mshindi lakini gura ni kufukuzwa mahali.
C. Pato ni chumo litokanalo na kazi na bato ni bamba la chuma lenye mikunjo.
D. Chura ni aina ya mnyama lakini jura ni kufanya jambo lisilo la kawaida.

30. Ikiwa mtondogoo itakuwa Jumanne, juzi ilikuwa
A. Alhamisi
B. Jumanne
C. Jumatano
D. Ijumaa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Alipojiunga na kidato cha kwanza, Mwakavu alikuwa wembe masomoni. Aliposajiliwa, walimu walifurahi ghaya kwa kumpata mwanafunzi aliyeonekana kuwa tumaini la shule yao. Kila aliyeziona alama alizopata katika mtihani wa mwisho wa shule ya msingi aliachwa kinywa wazi. Walimu **walimpa mkono wa tahania** na kumwambia waziwazi kuwa walikuwa na uhakika angeiinua beramu ya shule yao.

Wanafunzi wenzake aidha waliisifu shule aliyotoka. Tayari walikuwa wanalijua jina lake kwa kuwa lilikuwa limechapishwa magazetini. Mwakavu alikuwa miongoni mwa watahiniwa mia bora nchini. Kutokana na sifa hizi, walimstahi na kumcha. Pamoja na kufasili kuwa jina lake liliashiria jinsi alivyowashinda, walimbandika lakabu 'komesha' kwa vile walisadiki angewakomesha kimasomaso hadi afike kidato cha nne. Waliamini angekwangura takriban alama zote katika mtihani wa kidato cha nne.

Baada ya siku kadhaa shuleni, kila mmoja alimjua kwa jina na sura. Wakamwenzi Mwakavu. Hata hivyo, alipojua kuwa anamiminiwa sifa kochokocho, alianza kujishaua na kutembea mabega juu. Wanafunzi waliopata alama za juu walitaka kuhusishwa naye na kuwa wandani wake ili awaelekeze masomoni. Waliokuwa mbali naye walijitanibu naye kwa kumwogopa.

Kwa kujua sifa kemkem alizolimbikiziwa, Mwakavu aliamini kuwa shule ya upili ilikuwa mahali pa kupitia tu. Aliamini lazima angewafyokocha wenzake wote mosomoni. Alisubiri tu miaka minne ipite ili aorodheshwe tena katika magazeti miongoni mwa watahiniwa bora. Hakuona haja ya kutia bidii. Aliwaona wenzake kama visu vilivyosenea. Aliwasikiliza tu walimu darasani bila hata kunakili waliyokuwa wakifunza. Si mambo aliyofunzwa yalikuwa mboga kwake? Wakifunzwa, mara kwa mara alikuwa akisoma mambo yasiyohusiana na masomo.

Kwa kujihisi kuwa wanafunzi wa wastani, wenzake walijizatiti. Waling'amua kuwa kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Walipofanya mtihani wa muhula wa kwanza, wote walitarajia Mwakavu awakomeshe. Kwa mshangao wa wengi, alikuwa nambari kumi. Jambo hili liliangaliwa kwa fasili tofauti: Kwa wanafunzi waliomshinda au kumkaribia, ulikuwa mwanga wa matumaini yao. Walimtumia kama tayu ya kujipimia uzani wao kimasomo. Kwa walimu-ulikuwa mshangao - walilotarajia halikuwa. Kwake mwenyewe, ilikuwa fursa nyingine ya kujishaua-alifurahi kuwa licha ya kutokuwa makini wala kudurusu, alishindwa na wanafunzi tisa pekee. Alisahau papo kwa papo kamba hukata jiwe.

Walimu walimjadili, wakamchunguza na kujua udhaifu wake, wakaamua kumsaidia. Alipewa ushauri anuwai, kwa mfano, awe akinakili mafunzo, kushiriki midahalo na kufanya mazoezi ya ziada. Haya yote yalikuwa mbegu iliyoanguka mwambani, ikakosa kuota. Aliendeleza purukushani zake na kusema kuwa mitihani ya mihula ni lele tu. Kwake ngoma yenyewe ikifika angeicheza hadi wote washangae. Alisikika akisema mara kwa mara, 'Imara ya jembe kaingoje shambani'. Akakaidi yote aliyousiwa.

Jinsi mihula ilivyoyoyoma ndivyo alivyoendelea kudorora. Hatimaye alididimia dididi. Matumaini kwamba angegeuka mwanga wa shule yaligeuka kiza kilichotisha. Kwa kuongozwa na wa kale waliosema kuwa "Mcheza hawi kilema ngoma yataka matao," wenzake waliendelea kujikakamua.

Walipofika kidato cha nne, aliyejulikana sasa miongoni mwa mwanafunzi wenzake kwa jina, Mwakavu bin mchapo, **alikuwa akiona karibu kisogo cha kila mwanafunzi**. Jitihada za walimu walioshirikiana kwa muda mrefu na wazazi wake sasa zikawa zimetemewa mate. Ajabu ni kuwa haukumpiga mshipa . Aliamini kuwa werevu wake ungemsaidia kusoma katika mihula miwili ya mwisho na kuwapiga mwereka wenzake.

Kutanabahi, alikuwa ametaahiri mno. Mtihani wa kidato cha nne ulikuwa unamjia kwa kishindo. Kila siku ya muhula wa tatu ilikuwa ikimdhihaki. Mkosefu wa kitoweo humagiria. Alijaribu kusoma vitabu vya kiada lakini yaliyokuwemo yalikuwa kitendawili. Akagundua kuwa maelezo ya mwalimu ni muhimu kwa kuwa huyaeleza yaliyo vitabuni kwa wepesi na kumwelekeza mwanafunzi. Hapakuwa na muda wa kuwaendea walimu. Mtihani ulimgumbika. Matokeo yake yalikuwa malipo kamili, sawasawa na matendo yake.

31. Kulingana na aya ya kwanza
A. walimu walishangazwa na matokeo mazuri aliyopata Mwakavu
B. Mwakavu alikuwa mwanafunzi mwenye uwezo wa wastani shuleni
C. Mwakavu alikuwa mwanafunzi bora zaidi katika shule yake ya msingi
D. walimu walimtarajia Mwakavu kuliinua jina la shule yao.

32. Maelezo yapi si kweli kumhusu Mwakavu?
A. Jina lake lilichangia zaidi katika ufanisi wake masomoni.
B. Alikuwa miongoni mwa wanafunzi bora zaidi nchini katika mtihani wa shule ya msingi.
C. Aliiletea shule yake ya msingi sifa kochokocho.
D. Wapo wanafunzi waliomwogopa kutokana na uwezo wake katika masomo.

33. Kusifiwa kwa Mwakavu shuleni kulimfanya
A. awe dhaifu kielimu
B. apendwe na wote shuleni
C. awe mwenye kiburi
D. aimarike masomoni.

34. Matokeo ya Mwakavu yaliathiriwa na yote haya isipokuwa
A. kufanya shughuli mbadala wakati wa vipindi vya darasa
B. kukosa maelekezo aliyohitaji aweze kujiboresha
C. kupuuza ushirika wa wenzake katika masomo
D. kutojua umuhimu wa kufanya maandalizi kwa wakati ufaao.

35. Wanafunzi waliosoma pamoja na Mwakavu
A. walithamini ushirikiano
B. wote walikuwa mabingwa
C. walimpuuza kwa mienendo yake
D. waliogopa kumshinda masomoni.

36. Uwepo wa Mwakavu ulikuwa na manufaa gani kwa wanafunzi wenzake?
A. Aliwaelekeza masomoni ili nao waweze kujiinua.
B. Walikuwa na uhakika wa kumshinda katika masomo.
C. Aliingiliana vyema na wanafunzi mbalimbali shuleni.
D. Waliweka malengo yao kwa kujilinganisha na uwezo wake kielimu.

37. Kauli '**Alikuwa akiona karibu kisogo cha kila mwanafunzi**' ina maana gani?
A. Alikuwa mwanafunzi wa mwisho darasani.
B. Aliwashinda wanafunzi wachache sana darasani.
C. Alikaribiwa kimasomaso na wanafunzi wengi darasani.
D. Aliwashinda takriban wanafunzi wote darasani.

38. Kulingana na aya ya mwisho, Mwakavu
A. alianza kuimarika katika muhula wake wa mwisho
B. hakufanya jitihada zozote hadi mwisho
C. alichelewa kugundua mchango wa mwalimu masomoni mwake
D. alipata matokeo yaliyolingana na yale ya hapo awali.

39. Methali gani haiwezi kutumiwa kuelezea maisha ya Mwakavu?
A. Mpanda ovyo hula ovyo.
B. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji.
C. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.
D. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

40. Msemo '**walimpa mkono wa tahania**' jinsi ulivyotumika una maana ya
A. walimpongeza
B. walimsifu
C. walimtuza
D. walimkashifu.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Waja wengi hawawezi kunywa chai au uji bila kutia sukari. Wanaitumia sukari kwa hamu na ghamu bila kumaizi kuwa hiyo ni sumu wanayojiongezea mwilini. Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wetu wa jadi waliishi kwa muda mrefu wakiwa na **rai** murua kuliko sisi. Hii ni kwa kuwa waliishi katika enzi ambazo sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. Iwapo ilikuweko, ilikuwa bidhaa ya wateule waungwana na akina yahe wasingeweza kuigharimia.

Watafiti wa masuala ya afya wamegundua kuwa sukari inayotengenezwa viwandani sasa hivi haina virutubishi vyovyote. Umuhimu wake ni kutia ladha tamu tu. Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii. Baada ya kusagika mwilini, sukari hii huacha masazo ya asidi mwilini yenye sehemu inayoathiri afya. Halikadhalika, utaratibu wa viwandani wa kutayarisha sukari ili iwe nyeupe na kuichuja huharibu virutubishi vinavyoweza kuwa muhimu mwilini.

Matumizi ya sukari kwa wingi husababisha madhara mbalimbali mwilini. Kwanza, huchangia kuoza na kuharibika kwa meno. Pili, sukari nyeupe imehusishwa na ongezeko la maradhi ya kisukari, moyo na hipoglisimia au upungufu wa sukari mwilini. Matumizi ya **kiholela** ya sukari huleta kipandauso ambao ni ugonjwa wa ghafla wa kuumwa pande mmoja wa kichwa unaoambatana na kichefuchefu, kutapika na matatizo ya kuona. Pili, huleta maradhi ya ngozi na figo, pamoja na ongezeko la kolestroli. Kemikali hii inaporundikana moyoni, hufanya mishipa inayotoa damu moyoni na kuisambaza mwilini kuwa miembamba na sugu. Moyo hulazimika kusukuma damu kwa nguvu na huenda ukachoka na kukoma kufanya kazi.

Madhara haya ya sukari ndiyo yanayowafanya watu wengi kukiri kuwa **sukari, ingawa ni tamu, ina sumu mwilini**. Wataalamu wa maakuli wamependekeza ulaji wa vyakula kama nafaka, matunda, mboga na miwa ambavyo vimejaa sukari asilia.

Fauka ya hayo, sukari inayotoka katika asali ni bora zaidi katika mwili wa mwanadamu. Asali huwa na sukari asilia, vitamini, madini na amino asidi. Hivyo vyote huunufaisha mwili kwa njia ainati. Mathalani, asali huupa mwili nguvu zinazohitajika kuendesha shughuli za viungo. Licha ya hayo, asali huchangamsha mwili. Aidha, huwa na kemikali ambazo huwasaidia watoto kukua vizuri. Huweza kuzidisha kiwango cha himoglobin, hivyo kupunguza uwezekano wa watoto kuwa na anemia. Halikadhalika, asali husaidia katika usagaji wa vyakula iwapo itatumiwa kabla ya mlo. Matumizi ya kijiko kimoja cha asali kila siku husaidia mwili kujikinga dhidi ya maradhi ya kukohoa. Aidha, husaidia kuondoa harufu mbaya kinywani.

Vilevile, asali inaweza kutumiwa kujipaka. Inapotumiwa kwa njia hii hutunza ngozi na kuifanya ing'ae, huondoa vipele na ugumu wa ngozi, pamoja na kutibu kule ngozi ilikokatikakatika. Aidha, asali hutibu vidonda. Viwanda vingi vya vipodozi hutumia asali kama malighafi muhimu ya kutengenezea bidhaa hizo.

**41.** Watu wengi hawawezi kutumia chai au uji bila sukari kwa sababu
A. wanayajua madhara yake
B. wanaijua thamani yake
C. hawayajui madhara yake
D. hawaijui thamani yake.

**42.** Wazee wa zamani waliishi miaka mingi kwa sababu
A. hawakutumia sukari enzi hizo
B. kulikuwa na huduma bora zaidi za afya
C. hakukuwa na sukari enzi zao
D. walitumia aina ya sukari isiyo na madhara.

**43.** Chagua jibu lililo sahihi.
A. Uhaba wa pesa ulifanya baadhi ya watu wasitumie sukari.
B. Wenye matendo ya kiungwana ndio walioruhusiwa kutumia sukari.
C. Akina yahe waliwekewa vikwazo sukari inayotengenezwa viwandani haikuwa rahisi kupatikana.
D. Sukari inayotengenezwa viwandani haikuwa rahisi kupatikana.

**44.** '**Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii**'. Maana yake ni kuwa
A. watu wanaupendelea utamu wa sukari hata kama ina madhara
B. utamu huu si kitu yakizingatiwa madhara ya sukari hii
C. madhara haya si chochote yakilinganishwa na utamu wa sukari yenyewe
D. haijalishi inavyotumiwa sukari hii kwani ina madhara mengi.

**45.** Ni kauli ipi isiyo sahihi kulingana na ufahamu?
A. Matumizi ya sukari ya viwandani husababisha madhara mengi mwilini.
B. Sukari ya viwandani husababisha asidi katika mwili.
C. Ulaji wa vitu vya sukari nyingi huathiri meno kwa njia hasi.
D. Matumizi ya sukari nyeupe huchangia upungufu wa sukari mwilini.

**46.** Matumizi '**kiholela**' ni sawa na
A. bila kujali
B. kwa vyovyote vile
C. bila mpango
D. kupita kiwango.

**47.** Moyo ni kiungo kinachosukuma damu mwilini. Ni kiungo kipi husafisha damu mwilini?
A. Kibofu
B. Mishipa
C. Kongosho
D. Buki.

**48.** Vyakula vya nafaka, mboga, matunda na miwa vinafaa zaidi kwa kuwa
A. havina sukari yoyote
B. vina sukari nyingi zaidi
C. vina sukari asilia isiyodhuru
D. vinatosheleza afya kikamilifu.

**49.** Kifungu hiki kimetaja manufaa mengi ya asali. Yapi si kati ya manufaa hayo?
A. Kukinga mwili dhidi ya maradhi.
B. Kuimarisha usagaji wa nafaka.
C. Kuboresha ukuaji wa watoto.
D. Kuimarisha ngozi ya binadamu.

**50.** Kichwa mwafaka zaidi kwa makala haya ni
A. Umuhimu wa sukari mwilini.
B. Namna ya kudumisha afya bora.
C. Aina za vyakula vya sukari.
D. Madhara ya sukari nyeupe.

Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu ukifuata maagizo uliyopewa.

Andika hotuba iliyotolewa na kiranja wa shule yenu katika karamu ya kutuza wanafunzi walioibuka washindi katika mtihani wa mwisho wa muhula akihimiza jinsi ya kufaulu masomoni.